# Wakati ni Mali


## sekunde, dakika na masaa




Siku moja asubuhi Kibena, Kiduchu, Koba na Baraka walikutana kuwapangia wanyama wa Kokotoa mashindano ya kukimbia.




Mama Ndege, Ngedere, Toto Tembo,
Da Chura, Anko T and Kaka Kobe walisimama
kwenye mstari wakijitayarisha kushindana.



Koba aliwaonyesha ramani ya njia. Kwenye ramani kulikuwa na miti na njia iliyozunguka mwanzoni na mwishoni, na vizuizi kama mito na vilima.



Aliwaambia wanyama waisome ramani ili wasipotee.



Anko T alisema hakuhitaji ramani maana aliweza kuona njia nzima kwa kuangalia juu ya miti.



Aliweza kumwona Kiduchu akisimama mwishoni karibu na saa ya digitali.



Watoto walimuuliza
Kaka Kobe kama anataka
wamwinue juu ili aone
njia vizuri lakini alikataa.



Jua lilianza kuwa kali sana.
Koba aliwaambia wote
wajitayarishe kuanza.



Alitazama saa yake akasema mashindano ya kukimbia yataanza saa moja kamili.



Alihesabu chini kuanzia
tatu...mbili...moja,
akapiga filimbi kuanzisha
mashindano.



Kiduchu aliposikia sauti ya filimbi alianzisha saa ya digitali. Ilikuwa na sehemu tatu... Masaa: Dakika: Sekunde



Wanyama wakaanza kukimbia.



Mara Mama Ndege aliruka juu na kupaa kwa haraka juu ya miti, kwa mwendo wake aliwaachia wengine wote nyuma.





Ngedere alibembea
kwenye matawi ya miti.



Anko T, Toto Tembo na Da Chura
walikimbia kwa kasi kadri
ya uwezo wao.

Anko T alimpita Toto Tembo, lakini Toto Tembo hakuweza kumfuata kwa mwendo wake kwa ajili ya miguu yake mifupi.



Da Chura alishika mkia
wa Toto Tembo
na kufurahia ujanja wake.



Kwa ghafla, Mama Ndege aliruka kupitia mstari wa mwisho na kuvunja utepe.



Saa ilionyesha sekunde hamsini na nane.
“Kumbe, Mama Ndege,
una kasi kweli!”
Kiduchu alisema.




Saa iliendelea.


Baraka hakuelewa kwa nini namba za sekunde zilirudia sifuri na kuanza kuhesabu tena.



Aliwaita wengine,
kuwajulisha saa imeharibika.
“Haijaharibika,
inafanya kazi vizuri,”
Kibena alimwambia.




“Ona ina sehemu tofauti.
Kuanzia upande wa kulia kwenda kushoto inaonyesha sekunde
dakika
masaa.



Kwa sababu kuna sekunde sitini kwenye kila dakika,
sekunde zilihesabia hamsini na tisa,




halafu zilianzia sifuri tena,
wakati dakika iliongezeka moja.






Unaona sehemu ya dakika inaonyesha “moja” sasa,




Na sekunde zimeongezeka
“kumi na mbili” kutoka “sifuri.”

Inaendelea hivyo. Baada ya kila sekunde sitini, dakika zinaogezeka moja...

**sekunde 60 = dakika 1**

Na dakika zinaendelea kuongezeka hivyo...



Pia, kwenye kila saa kuna dakika sitini.


**dakika 60 = saa 1**

Maana baada ya
dakika hamsini na tisa,

tutapata “saa moja” kwenye
sehemu ya masaa...
na dakika zitarudia
sifuri na kuanza tena.



Endelea kuangalia saa mashindano yakiendelea. Utaona jinsi saa inavyofanya kazi utaelewa."



Baraka alikubali akaanza kurudia tena na tena,
“Sekunde sitini ni sawasawa na dakika moja.

**sekunde 60 = dakika 1**

Dakika sitini ni sawasawa na saa moja.”

**dakika 60 = saa 1**







Wa pili kupita mstari wa mwisho alikuwa Ngedere. Alibembea akiwapitia, akageuka angani na kushuka.

Ilimchukua dakika nne na sekunde ishirini na tano.



Alishangaa kusikia ameshindwa na Mama Ndege.
Alikuwa na uhakika atashinda kwa kubembea.




Baada ya muda, Anko T alifika akihema kwa ngumu. Alichoka sana kwa hiyo alinyosha shingo yake ikapite mstari wa mwisho.




Alipata dakika thelathini na moja
na sekunde thelathini na sita.



Wakati huo Toto Tembo alikuwa anakimbia haraka kadri alivyoweza bila ya kujua Da Chura alikuwa amening'inia mkiani mwake.



Alipokaribia mstari wa mwisho,
Da Chura aliruka juu ili apite mstari na
kushuka mbele ya Toto Tembo.




Saa ilionyesha kwamba Da Chura alichukua

saa moja | dakika arobaini na saba | sekunde ishirini na nne.



Muda wa Toto Tembo ulikuwa

saa moja, dakika arobaini na saba sekunde ishirini na tano.










Da Chura alimshinda kwa sekunde moja tu!


Toto Tembo alilalamika kuwa haikuwezekana ameshindwa na Da Chura kwa sababu hakumwona akimpita njiani. Hakujua alipata lifti bure mkiani mwake!



Toto Tembo alilalamika kuwa haikuwezekana ameshindwa na Da Chura kwa sababu hakumwona akimpita njiani. Hakujua alipata lifti bure mkiani mwake!



Toto Tembo alijaribu kutazama mkia wake lakini hakuweza kumwona Da Chura. Alitingisha mkia wake ili Da Chura aruke mbali. Wote walicheka.



Kiduchu alisimamisha saa
na Baraka alitangaza
Mama Ndege ndiye mshindi.



Ndege wote walimshangilia kwa nguvu. Mama Ndege aliinamisha kichwa chake kuwashukuru wote.



Anko T alidakia, “Mimi ni mshindi kwa kweli.
Wao hawakukimbia kwa miguu.





Mama Ndege aliruka na Ngedere alitumia matawi.
Hayo yalikuwa mashindano ya kukimbia,
na mimi nilikuwa mkimbiaji wa kwanza. Niwe mshindi!”

Toto Tembo alikubaliana na Anko T, akasema awe mshindi wa pili kwa sababu alikuwa mkimbiaji wa pili.




Ngedere alidai Da Chura alimshinda
Toto Tembo, kwa hiyo Da Chura awe
mshindi wa pili na Toto Tembo awe wa tatu.





“Sio kweli! Da Chura
alipata lifti kwa kushika mkia wangu!”
Toto Tembo alisema.

Mama Ndege aliongeza, “Sikusikia sheria zozote zilizohusu kutoruka. Unafikiri kuruka ni rahisi? Basi wewe ujaribu.”



“Au jaribu kubembea kwa matawi,” Ngedere alisema akiwaonyesha lengelenge mikononi mwake.



“Basi mimi nadai nimeshinda kwa sababu nilikuwa wa kwanza kuona mstari wa mwisho. Kuona kwangu ni haraka kuliko kuruka na kubembea kwenu!” Anko T alisema.



Wakati wanyama walikuwa wanagombana, Kaka Kobe aliwafikia kwa kimya na kujitupa kwenye utepe wa mwisho.



Alilia kwa sauti gamba lake lilipogusa ardhi. Watoto walimsogelea kuhakikisha hajaumia. Walikuwa wamemsahau kwa ajili ya mwendo wake wa polepole.



“Kaka Kobe amekuwa wapi kwa muda wote huu?” Da Chura aliuliza akicheka.



Kaka Kobe alichoka sana, hakuweza kuongea. Alipopata nguvu tena aliiulizia ajue muda wake.



Mwaka uliopita alichukua

masaa mawili dakika thelathini na mbili.




Sasa alitaka ajue kama alivunja rekodi yake ya mwaka jana!


Kibena alimwomba awasamehe, maana hawakujua muda aliotumia kwa sababu walishasimamisha saa.



Koba alisema kwamba wataweza kuikokotoa.



“Kaka Kobe alimaliza saa tatu na dakika ishirini.




Mashindano yalianza saa moja kamili.



| | Masaa | | Dakika |
|---|---|---|---|
| | 03 | : | 20 |
| − | 01 | : | 00 |



Tunahitaji kukokotoa utofauti kati ya saa moja na saa tatu na dakika ishirini.
Inabidi tutoe,” Kibena alisema.



"Tuanze na dakika,

| | Masaa | | Dakika |
|---|---|---|---|
| | 03 | : | 20 |
| − | 01 | : | 00 |
| | 02 | : | 20 |

Sifuri toa sifuri ni sifuri.

Mbili toa sifuri ni mbili.

Sasa ona masaa hapa.
Tatu toa moja ni mbili.

Jibu ni masaa mawili na dakika ishirini."

Kibena alimwambia Kaka Kobe kwamba mwaka huu alichukua masaa mawili na dakika ishirini kukimbia umbali sawasawa na mwaka jana.





“Nikokotolee tafadhali! Nimeipunguza muda wangu kwa dakika ngapi?” Kaka Kobe alimuuliza.




"Ili tujue umeenda kwa kasi gani zaidi kuliko mwaka jana, inabidi tujue tofauti kati ya



muda wa Kaka Kobe mwaka jana



na muda wake leo.

Tuanze na dakika.

| | Masaa | | Dakika |
|---|---|---|---|
| | 02 | : | 32 |
| − | 02 | : | 20 |
| | | | 12 |

Tutoe.

Mbili toa sifuri ni mbili.

Tatu toa mbili ni moja.



Sasa tukokotoe masaa.

| | Saa | | Dakika |
|---|---|---|---|
| | 02 | : | 32 |
| − | 02 | : | 20 |
| | 00 | : | 12 |

Mbili toa mbili ni sifuri.
Sifuri toa sifuri ni sifuri.

Utofauti kati ya muda wako mwaka uliopita na muda wako mwaka huu ni dakika kumi na mbili."

Kibena alimwambia Kaka Kobe kwamba
aliboresha muda wake
kwa dakika kumi na mbili,
inamaanisha alikimbia kwa haraka zaidi.



Kaka Kobe alisimama akaanza
kurukaruka kwa furaha.
Kisha akajitupa ardhini
kwa kuchoka.




Mama Ndege alimfurahia sana. Akamwambia,
“Anayekataa kushindwa ndiye mshindi.
Sisi tunagombania nani ni mshindi,
nani alikimbia kwa ukweli na nani
anastahili ushindi gani, wakati Kaka Kobe
anafurahia kuboresha muda wake tu.
Anayeboresha muda wake ndiye mshindi.”





"Asante, Mama Ndege...
lakini nahitaji maji sana,"
Kaka Kobe alisema.



Kwa bahati mbaya, hakukuwa na maji
yoyote mahali walipokaa. Walimfuata
Mama Ndege kuelekea mto ulio karibu nao.
Yalikuwa mashindano mazuri
na siku nzuri kwa wote.



# Mwisho

## Imeandaliwa na

## ubongo.co

Haki zote zimehifadhiwa.
Hairuhusiwi kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki kwa njia
ya aina yoyote bila idhini ya mwandishi,
UBONGO INTERNATIONAL.